



Walikuja watu kutoka khabila la Ukli au Uraina, wakauchukia mjini Madina

Imepokelewa kutoka kwa Anas bin Maalik -radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-amesema: Walikuja watu kutoka khabila la Ukli au Uraina, wakauchukia mjini Madina, kwa sababu hali ya hewa ya Madina haikuwafaa. Mtume rehema na amani ziwe juu yake akawaamuru waende katika ngamia wa zaka na wanywe mikojo yake na maziwa yake.

Wakaondoka, na baada ya afya yao kurejea, wakamuua mchungaji wa ngamia wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake na wakaiba ngamia hao. Habari zikamfikia

Mtume rehema na amani ziwe juu yake mapema asubuhi, basi akatuma watu kuwafuutilia, na wakapatikana kabla ya mchana. Mtume rehema na amani ziwe juu yake akaamuru mikono na miguu yao ikatwe, macho yao yakachomwa moto, na wakatupwa kwenye jangwa la mawe (Al-Harra). Wakawa wakiomba maji, lakini hawakupewa. Abu Qilaba anasema: Watu hawa walifanya wizi, wakafanya mauaji, walitoka katika Uislamu baada ya kuwa Waislamu, na walitangaza vita dhidi ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake.

[Sahih] [Wamekubaliana Bukhaariy na Muslim]

Walikuja watu kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, kutoka katika khabila la Ukli na Uraina wakiwa ni Waislamu, wakapatwa na ugonjwa na maradhi mazito kwao, yakavimba matumbo yao, wakachukia kuishi Madina kwa sababu chakula hakikuwapendeza wala hali ya hewa. Mtume rehema na amani ziwe juu yake akawaamuru waende katika ngamia za sadaka, na wanywe mikojo na maziwa yake. Wakaenda, na walipopona, na wakanenepa, na rangi zao zikarejea kuwa nzuri, wakamuua mchungaji wa ngamia wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, na wakachukua ngamia. Habari hiyo ilifika asubuhi na mapema, ndipo Mtume akatuma kikosi cha kuwafuata. Wakawakamata, wakati wa jua kupanda juu wakaletwa wakiwa mateka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake. Mtume akaamuru mikono yao na miguu yao ikatwe, na macho yao yakatobolewa, kwa sababu walimtendea hivyo mchungaji. Kisha wakatupwa kwenye eneo lenye joto (al-Harra), wakawa wakiomba maji lakini hawakupewa mpaka walipokufa. Amesema Abuu Qilaba: Ni kwamba wao waliiba, na wakaua, na wakakufuru baada ya imani yao, na wakampiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

النّجّات الخيريّة
ALNAJAT CHARITY

